

# S O M I C O V I D - 1 9



## Somo la COVID-19

COVID-19 ni **ugonjwawa mfumo wa kupumua** unaosababishwa na **kirusi** kinachoitwa Kirusi cha Korona. Kufahamu mengi kuhusu COVID-19 kunaweza kutusaidia kuwa salama na kuwalinda wengine.

MSAMIATI	Tafuta maneno haya katika somo hili
Kirusi	Kiini au kitu kidogo sana kilicho na uhai kinachosababisha ugonjwa
Mfumo wa kupumua	Viungo vya mwili vinavyokusaidia kupumua, kama vile mapafu
Tandavu	Ugonjwa unaoenea katika nchi nyingi au dunia nzima
Dalili	Ishara za ugonjwa kama vile kukohoau joto kali
Kuambukizwa	Kuwa mgonjwa
Kueua	Kusafisha kwa alkoholi au kipaushi ili kuua viini
Karantini	Kukaa nyumbani/ kujiweka mbali kutoka kwa watu wengine ili kukomesha kuenea kwa ugonjwa

### JE, DALILI ZA COVID-19 NI GANI?



Dalili zinaweza kuwa hafifu au kali zaidi na zinaweza kujitekeza kwa muda wa siku 2-14 baada ya kumkaribia mtu aliye mgonjwa.

Unapaswa kupimwa COVID ikiwa unazo dalili **hizi**.

Unapaswa kujiweka **karantini** wakati unangoja matokeo ya vipimo.

Unapasha kujiweka **karantini** kwa angalau siku 14 ikiwa vipimo vitaonyesha kuwa una maambukizi.

**TAMBUA:** Mtu aliyeambukizwa anaweza KUKOSA dalili lakini bado anaweza kukupa hivi virusi. Hiyo ndiyo sababu tunahitaji kuwa waangalifu tunapokuwa karibu na mtu yeyote.

### DALILI ZA DHARURA:

Ikiwa mtu anazo dalili hizi tafuta usaidizi haraka. Piga simu kwa 911 au nenda kwenye chumba cha dharura.

- Shida kupumua
- Maumivu au shinikizo lisilotulia kifuani
- Hawezi kuamka au kuwa macho
- Midomo au uso kuwa ya samawati

**JOTO KALI: Zaidi ya 100 F (38 C) inamaanisha unaweza kuwa uko mgonjwa.**

**JE COVID-19 HUENEA KWA NJIA GANI?**

- COVID-19 huenezwa hasa kutoka kwa mtu hadi mtu mwininge.
- Unaweza **kuambukizwa** kwa kumkaribia mtu aliyе na COVID-19: karibu futi 6 (**mita 2 au urefu wa mikono miwili**).
- Unaweza **kuambukizwa** kutokana na **matone ya hewa** (matone madogo yaliyo ndani ya hewa) wakati mtu aliyе mgonjwa anakohoa, kupiga chafya, au anapoongea.
- Unaweza kuupata kwa **kugusa sakafu** au kitu kilicho na virusi hivyo juu yake, na kisha kwa kugusa mdomo wako, pua, au macho.

**JE, NINAWEZA KUJILINDA VIPI PAMOJA NA WENGINE?**


The grid consists of six panels, each containing an illustration and a caption in Swahili:

- Futi 6:** Illustration shows two people maintaining social distance. Text: "Kaa angalau futi 6 (karibu urefu wa mikono 2) kutoka kwa watu wengine."
- Funikia:** Illustration shows a person covering their nose and mouth with a tissue. Text: "Funikia kukohoa kwako au kupiga chafya kwa tishu, kisha tupa hiyo tishu katika jaa la taka na kunawa mikono yako."
- Saidia Kujilinda Mwenyewe na Wengine:** Illustration shows three people wearing masks. Text: "Ukiwa ikutokana na COVID-19 vaa barakoa juu ya pua na mdomo wako".
- Osiguse macho:** Illustration shows hands being washed with soap. Text: "Osiguse macho, pua na mdomo wako".
- sakafu zinazoguswa mara kwa mara:** Illustration shows a hand spraying disinfectant. Text: "kueua vitu na sakafu zinazoguswa mara kwa mara."
- Kaa nyumbani ukiwa mgonjwa:** Illustration shows a person in bed inside a house. Text: "Kaa nyumbani ukiwa mgonjwa, isipokuwa unapoenda kutafuta huduma ya matibabu."
- Nawa mikono:** Illustration shows hands being washed with soap. Text: "Nawa mikono [cdc.gov/coronavirus](https://cdc.gov/coronavirus) kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20."



**Coronavirus ni nini, na unawezaje kukaa salama?**

<https://www.youtube.com/watch?v=dCIRfAVDkQM>



**Acha Kuenea kwa COVID (Kiingereza)**

## *Somo la COVID-19*

### *Mazoezi ya Masomo*

#### **LINGANISHA /TAMBUA /ANDIKA**

Je, ni mambo gani sita unayoweza kufanya ili kujilinda mwenyewe na wengine pia kutokana na virusi?

1.



Kaa nyumbani unapokuwa mgonjwa.

2.



Eua sakafu unazo gusa mara kwa mara.

3.



Nawa mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20.

4.



Usiguse macho, pua au mdomo wako.

5.



Vaa barakoa unapokuwa kwa umma.

6.



Kaa angalau futi 6 (urefu wa mikono 2) kutoka kwa watu wengine.

#### **JADILI**

Fikiria kuhusu yale ulijifunza kuhusu kudumu salama na mwenye afya wakati wa tandavu. Toa ushauri wako kuhusu moja ya hali zifuatazo. Jadili na kikundi au mwalimu wako.

Juan anafanya kazi ya kuvuna nyanya kondeni. Kila asubuhi anapaswa kuabiri gari ili kuenda kazini. Gari hilo limefurika sana kwa wafanyakazi wengine. Je, anapaswa kufanya nini ili kujilinda yeye na wengine pia?

Anapaswa \_\_\_\_\_.

Nancy ni mama wa watoto wawili wachanga. Anajaribu kukaa nyumbani kadri iwezekanavyo kwa sababu ya virusi hivi. Lakini saa zingine anahitaji kuenda nje dukani. Je, anaweza kufanya nini ili kujilinda mwenyewe, watoto wake, na watu wengine salama kutokana na virusi?


Anapaswa \_\_\_\_\_.

## *Somo la COVID-19*

### *Ratiba ya Masomo*

Nyenko
✓ Somo
✓ Kurejelea video
✓ Ukurasa wa Zoezi la Mwanafunzi
✓ Jaribio la Kabla / Jaribio la Baadaye

Vipengele	Mazoezi
Jaribio la Kabla	<ul style="list-style-type: none"> <li>Peana Jaribio la Kabla.</li> </ul>
Utangulizi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Eleza kuwa ni muhimu kujua mengi kuhusu virusi hivi ili kwamba tuweze kujisaidia wenyewe na wengine kudumu wenyewe afya.</li> </ul>
1. Msamiati na kufahamu virusi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Rejelea na utoe maelezo kuhusu msamiati wa somo hili katika kisanduku kilichoko juu ya ukurasa wa 1.</li> <li>Kwa ufanuzi, tumia maneno ya msamiati huu katika sentensi nyingine k.v. <b>“Dalili za virusi hivi ni....”</b></li> <li>Chunguza uelewa kwa kumuuliza mwanafunzi kutoa mfano wa kila neno.</li> </ul>
2. Dalili na Kuenea	<ul style="list-style-type: none"> <li>Soma kuhusu dalili na kuenea kwa virusi hivi.</li> <li>Hakikisha wanafunzi wanajua wakati wa kupimwa na mahali pa kuenda ili kupimwa COVID.</li> <li>Rejelea jinsi joto la mwili la kawaida linapaswa kuwa na wakati wa kutafuta usaidizi wa dharara.</li> </ul>
3. Je, ninaweza kujilinda vipi pamoja na wengine?	<ul style="list-style-type: none"> <li>Tazama michoro na usome taarifa kuhusu jinsi ya kujilinda mwenyewe na wengine pia.</li> </ul>
Rejelea	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ikiwa unafanya masomo kwenye kifaa cha kielektroniki, tumia video iliyopakuliwa ili kurejelea somo hili. Bonyeza maradufu kwenye video ili icheze.</li> <li>Ikiwa unaweza kupata intaneti unaweza kuchagua video ya ziada kwenye kiunganishi cha YouTube.</li> <li>Ikiwa unatumia karatasi na penseli, tazama nyuma kwenye somo ili kurejelea pointi muhimu.</li> </ul>
Mazoezi ya Masomo	<p><b>Zoezi la 1 Linganisha/Tambua/andika.</b> Muulize mwanafunzi kulinganisha maneno na picha na kutambua, na/au kuandika, kile wanaweza kufanya ili kujilinda wenyewe na wengine kutohakana na virusi.</p> <p><b>Zoezi la 2.</b> Soma kuhusu matukio yaliyopeanwa. Muulize mwanafunzi kutoa ushauri kuhusu kudumu salama na mwenye afya kwa mujibu wa kile wamejifunza katika somo hili.</p>
Jaribio la baadaye	<ul style="list-style-type: none"> <li>Peana jaribio la baadaye pamoja na swali la bonasi.</li> </ul>



## SOMO LA COVID-19

### JARIBIO LA KABLA

Jina: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

1. Futi sita ni urefu wa mkono mmoja kutoka kwa mtu mwingine.
2. Unaweza kupata virusi kutoka kwa mtu asiyekuwa na dalili.
3. Unaweza kupata virusi kwa kuvuta ndani matone yaliyo katika hewa.
4. Zaidi ya 100 F (38 C) inamaanisha unaweza kuwa uko mgonjwa.
5. Ili kuondoa viini unapaswa kunawa mikono yako kwa angalau sekunde 15-20.

Chora mviringo kwa jibu sahihi:

Ndio La

Ndio La

Ndio La

Ndio La

Ndio La

JUMLA YA YALIYO  
SAHIHI: \_\_\_\_\_



## SOMO LA COVID-19

### JARIBIO LA BAADAYE

Jina: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_

1. Futi sita ni urefu wa mkono mmoja kutoka kwa mtu mwingine.
2. Unaweza kupata virusi kutoka kwa mtu asiyekuwa na dalili.
3. Unaweza kupata virusi kwa kuvuta ndani matone yaliyo katika hewa.
4. Zaidi ya 100 F (38 C) inamaanisha unaweza kuwa uko mgonjwa.
5. Ili kuondoa viini unapaswa kunawa mikono yako kwa angalau sekunde 15-20.

Chora mviringo kwa jibu sahihi:

Ndio              La

Ndio              La

Ndio              La

Ndio              La

Ndio              La

JUMLA YA YALIYO  
SAHIHI: \_\_\_\_\_

Swali la bonasi kwa ajili ya Jaribio la baadaye: Taja baadhi ya njia za jinsi unaweza kujilinda mwenyewe kutokana na virusi:

- \_\_\_\_\_.
- \_\_\_\_\_.
- \_\_\_\_\_.

### Vyanzo

Taarifa ya somo hili kwa mujibu wa mwongozo wa Vituo vya Kudhibiti Magonjwa (CDC).

Michoro na video za somo hili kutoka kwa CDC na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Nebraska (Nebraska Department of Health and Human Services).



*Maudhui ya somo hili yalitayarishwa chini ya ruzuku kutoka Idara ya Elimu. Hata hivyo, maudhui haya hayawakilishi kwa vyoyote sera ya Idara ya Elimu, na hupaswi kudhania umeidhinishwa na Serikali Kuu.*